



**Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt Benilith Mahenge pamoja na viongozi wengine wakiwasili katika shule ya sekondari Manyoni kukagua ujenzi wa darasa ambalo ni miongoni mwa shule iliyoingia kwenye mradi wa fedha za uviko 19**



Viongozi wanaosimamia bodi za shule za Msingi na Sekondari pamoja na Madiwani katika kata mbalimbali Mkoani Singida wametakiwa kuwashirikisha wananchi katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ,Hospital,na Visima vya maji ili kukamilisha ujenzi huo kabla ya disemba 10, 2021.

Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt Benilith Mahenge ametoa kauli hiyo tarehe 8.11.2021 alipotembelea na kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari Manyoni ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kuhakikisha anasimamia na kuona miradi yote inatekelezwa kwa wakati kulingana na hizo la Mh Rais Samia Suluhu Hassani kwamba ifikapo desemba 10 ,2021 madarasa yote yawe yamekamilika .

Mkazo wa ushirikishwaji wa wananchi umewekwa baada ya Dkt Mahenge kutoridhika na utendaji wa kazi hizo za ujenzi kwa kutegemea mafundi pekee hali inayoweza kusababisha kukwama kabisa kwa miradi kukamilika kwa wakati.

“katika Wilaya nyingine wananchi wamehamasika ambapo walichimba misingi na kusaidia kukusanya mchanga ,kokoto na pia waliweza kubeba zege hali iliyosaidia kazi kwenda haraka

sasa hapa naona kuna mafundi tu hatuwezi kumaliza kazi hii kwa wakati tuhamasishe wananchi” alisema Dkt Mahenge.

Dkt Mahenge amesema mpango uliopo ni kuhakikisha vyumba vya madarasa kwa Sekondari na msingi shikizi kwa Mkoa wa Singida kukamilika kabla ya disemba 15, 2021 na amesema kuwa endapo itashindikana kukamilishwa kwa namna yeyote ile basi wasimamizi wanaohusika wajiandae kufukuzwa kazi.

Aidha amesema kuwa wadau wanaruhusiwa kuchangia baadhi ya v itendea kazi ikiwemo mchanga, kokoto, au kuongeza nguvu kazi kwakuwa kila darasa lilikadiriwa kutumia Tsh.milion.20.

Amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuhakikisha wananunua vifaa kwa pamoja ili kupunguza gharama ikiwa ni pamoja kutoa oda mapema kwakuwa mahitaji ni makubwa ambapo kila Mkoa vinahitajika .

Nataka mjiongeze hakutakuwa na msamaha kwa yeyote atakayesababisha wanafunzi kukosa madarasa wakati fedha tayari zimeshatolewa ,sihitaji kusikia eti vifaa viliisha ,ndiyo maana nasema mjiongeze mtoe oda mapema .alisisitiza Dkt Mahenge.

Naye. Alhaji Juma Kilimba Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida akawataka viongozi wote wa chama Mkoa ,Wilaya,Kata na Tarafa kuhakikisha wanasimamia na kuhimiza wananchi kushiriki nguvu kazi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata madarasa ifikapo disemba 15 mwaka huu.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa amesema kuwa wamejipanga vizuri na kwamba wameshagawa timu mbalimbali katika kila maeneo na kwamba yeye anatembelea hakai ofisini na anajitowa kuhakikisha anashiriki kwa mfano kuongeza nguvu kazi.

Halmashauri ya Manyoni pekee imepokea Zaidi Bilion 2.8 ambazo zinatazamiwa kujenga madarasa shule shikizi ni Bilion 1.na million 460, madarasa ya sekondari milioni 960, jengo la huduma za dharula mil.300 na Bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu tsh mil 80.

Katika ziara yake ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Mkuu wa Mkoa aliongozana na viongozi wa chama cha mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida Mh Mwenyekiti Alhaji Juma Kilimba, katibu wa chama cha mapinduzi Mkoa wa Singida, Muhandisi wa barabara tanroad Mkoa wa Singida na viongozi wengine.



Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt Benilith Mahenge kulia na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Manyoni Jumanne Mlagaza kushoto wakichanganya zege kujenga msingi wa darasa katika shule ya sekondari manyoni



viongozi wa ulinzi na usalama wa Wilaya ya Manyoni nao hawakuwa nyuma





kaimu Mkurugenzi Fadhili Chimsala naye alishiriki kuchimba msingi



Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Rahabu Mwangisa akishiriki katika uchimbaji wa msingi



Katibu Wa CCM Mkoa Bi Lucy Shee Naye Alishiriki Kukata Visiki



Dso Wilaya ya Manyoni Mpegwa Mwakasendo akichimba msingi





Mkuu wa Mkoa akijiandaa kushika sululu tayari kwa kuchimba msingi



Afisa elimu sekondari wilaya ya manyoni Ramla naye alishiriki kusomba zege